

Kumbuka

Unapohamisha mifugo kutoka sehemu moja hadi nyingine, pata kibali cha kusafirisha kutoka kwa serikali.



Mifugo wenye afya



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P 5781 I, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishaji:

Wesonga, H.O., Omondi, S.P., Musyoki, J., Omwenga,
S. na Mugambi, J.M.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo,

KARI Muguga North

S.L.P.32 Kikuyu,00902

Simu: (066) 32106/7,3200

Nukulishi: (066) 32450

Baruapepe: vrckari@yahoo.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 39 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Kutambua na kuzuia homa ya mapafu (Nimonia) ya ngombe (CBPP)




Utangulizi

Nimonia ya mifugo au *Contagious bovine pleuropneumonia* (CBPP) ni ugonjwa unaowaathiri mifugo. Jamii tofauti wanayo majina tofauti ya ugonjwa huu.

Majina Ya Kijamii	
Jamii	Jina La Kijamii
Kamba	Mavui
Somali	Sambap
Maasai	Olkipiei
Turkana	Loukoi

CBPP huambukishwaje?

Maambukizi hasa hutokea mfugo mwenye afya anapo karibiana na mfugo aliye na maradhi haya. Haya hutendeka malishoni, sokoni na sehemu wanapokunywa maji.



Mifugo waliokaribiana

Impact of CBPP

- Upungufu wa faida za kifedha kwenye jamii
- Ukosefu wa nguvu za fahali wa kulima
- Kutoweza kufanya tambiko zinazohusiana na mifugo
- Vizuizi vya kibiashara nchini na ng'ambo.

Ishara za CBPP

- Kuhema na kushindwa na kupumua.
- Kohozi kavu lililo ndani, baada ya kukimbia.
- Makamasi yenye damu.
- Mifugo kupoteza uzito na kuonekana wanyonge.
- Vifo vya ghafla.
- Shingo lililotokeza, miguu ya mbele kuachana na viuno vya miguu kutokea nje.



Shingo lililofutwa nje dalili ya CBPP

Matokeo Ya Upasuaji

- Mapafu yaliyojikita kwenye kabati la kifua.
- Kabati la kifua huenda ikawa na majimaji ya manjano.
- Mapafu yameangama (kama maini), yenye rangi nyekundu, au kijivu.
- Mapafu yenye sehemu zilizooza kule kumejikita (*sequester*).



Mapafu yenye alama alama

Uzuiaji na uangamizaji wa CBPP

kukiwa na maambukizo:

- Mkulima anapohisi uwepo wa homa ya mapafu, daktari wa mifugo aarifiwe mara moja.
- Daktari wa mifugo atachunguza na achukue majaribio zikachunguziwe kwenye chumba cha uchunguzi.
- Ng'ombe wote katika zizi lililoathiriwa hupimwa chini ya usimamizi wa serikali.
- Ng'ombe wote wenye maradhi ya CBPP huchinjwa.
- Serikali inatangaza kizuizi cha usafirishaji wa mifugo.
- Ng'ombe wasio na maradhi hupata chanjo na zizi zenye afya zilizoko kilomita 30 karibu na zizi lenye maradhi pia huchanjwa.
- Zizi lililoathiriwa hupimwa baada ya kila miezi 3 hadi kusiwe na matukio mapya ya maambukizo.

Kama Hakuna Maambukizo

- Chanjo zifanywe kulingana na maagizo ya wataalam wa mifugo walio karibu.
- Wacha nafasi ya mita mia moja au masafa katika ya mifugo yako na wale wanaopitia karibu nawe.